



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/74, Fax: +255222129878,
General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

Serikali imeandaa viwango na miongozo mbalimbali inayotoa maelekezo na ufafanuzi wa taratibu zinazotakiwa kuzingatiwa ili kuwa na matumizi sahihi na salama ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika hatua za kupanga, kubuni, kupata, kununua, kusimamia na kuendesha mifumo mbalimbali ya Tehama Serikalini.

Miongozo na viwango hivyo vinalenga kuziwezesha taasisi za umma kujenga mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya taasisi husika na kuepuka mifumo inayojengwa kwa shinikizo la wafanyabiashara, wafadhili au kwa matakwa ya mtu binafsi.

Aidha, inabainisha taratibu za kusanifu, kutengeneza na kuendesha mifumo inayowasiliana na kubadilishana taarifa miongoni mwa taasisi hizo ili kuboresha utoaji wa maamuzi na huduma kwa wananchi wanaoishi mijini na vijijini kwa haraka, gharama nafuu na kwa ufanisi mkubwa.

Pia, kwa kutumia miongozo na viwango hivyo, Serikali itakuwa na uwezo wa kuepuka urudufu wa mifumo na kupunguza gharama kubwa za uendeshaji na kuwa na mifumo endelevu na yenye gharama halisi na inayofuata viwango vya Usalama katika kulinda taarifa na data za Serikali.

Aidha, Miongozo na viwango vitapitiwa mara kwa mara na kuchapishwa kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, mahitaji ya shughuli na matakwa ya Serikali. Viwango na Miongozo hii inapatikana katika tovuti ya Wakala ya Serikali Mtandao www.ega.go.tz sehemu ya miongozo na viwango.

Hivyo, Wakala ya Serikali mtandao inashauri Taasisi zote za Umma ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekreterieti za Mikoa, Wakala za Serikali/Mamlaka, Bodi, Tume, Mabaraza, Mifuko, Mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuata miongozo na viwango vilivyotolewa katika uanzishaji na usimamizi wa mifumo ya Tehama Serikalini.

Vilevile, taasisi hizo zinashauriwa kuwasilisha maandiko ya mifumo mipya ya TEHAMA ili iweze kuthibitishwa iwapo imefuata miongozo na viwango vilivyowekwa kabla ya kujengwa na kusakinishwa. Aidha, taasisi hizo zinatakiwa kujaza taarifa za mifumo au miradi ya TEHAMA iliyopo katika mfumo wa kukusanya na kutunza taarifa za miradi ya TEHAMA Serikalini unaopatikana katika anuani ya <http://gip.ega.go.tz>

Pia, kwa wafanyabiashara wanaojihusha na miradi au utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini wanashauriwa kufuata miongozo na viwango hivi ili kujua mahitaji halisi ya Serikali na kuweza kujenga mifumo ya TEHAMA endelevu na inayoleta tija kwa umma.

Wakala ya Serikali Mtandao (e-Government Agency) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 2012 kwa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30, Sura ya 245 ya mwaka 1997. Wakala hii ina majukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania.

XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX **MWISHO**XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX

Imetolewa Na:
MTENDAJI MKUU
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)